



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 4, Issue 1, 2019

ISSN: 1476-4687

EANSO

EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

DHIMA YA UMAHULUTI WA UTAMADUNI KATIKA UAMILISHAJI WA NYIMBO ZA HARUSI MIONGONI MWA WANANDI

Jennifer Chepleting Koech¹, Dkt. Fred Wanjala Simiyu² & Margan Adero³

¹Catholic University of Eastern Africa, SLP 62157 – 00200, Nairobi, Kenya, jenniferchepleting@gmail.com.

²Kibabii University, SLP 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wsimiyu@kibu.ac.ke.

³Catholic University of Eastern Africa, SLP 62157 – 00200, Nairobi, Kenya, moduyah@gmail.com.

Article history:

Received: 01 Nov 2019

Accepted: 04 Nov 2019

Published: 15 Nov 2019

Keywords:

Umahuluti,
Utamaduni,
Uamilishaji,
Nyimbo,
Tumdo

IKISIRI

Wakenya wengi hushutumu suala la umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za wasanii maarufu nchini. Madai yao ni kuwa umahuluti wa utamaduni husababisha kupotea kwa utamaduni asili wa jamii mbalimbali za Wakenya na kuiga ule wa Wakoloni. Utafiti huu ulikusudia kuhakiki dhima ya umahuluti wa utamaduni katika uamilishaji wa nyimbo za harusi mionganii mwa jamii ya Wanandi nchini Kenya. Nadharia ambayo iliongoza utafiti huu ni ya ubaada ukoloni. Baadhi ya wahasisi wakuu wa nadharia hii ni Homi Bhabha, Gayatri Chakravorty Spinak, Edward Said, Robert Young na Bill Ashcroft. Mtafiti alipata data yake kuititia usaili na uchanganuzi wa yaliyomo kwenye vipindi vya Tumdo katika runinga ya Kass. Jumla ya wahojiwa nane walisailiwa kutoka kata ya Chepsaita, eneo la kaunti ndogo ya Turbo kwenye kaunti ya Uasin-Gishu. Idadi kubwa ya wakazi wa Uasin-Gishu ni Wanandi ambaao walihamia eneo hilo kutoka kaunti ya Nandi; kwa hivyo wameingiliana na jamii zingine wa hapa nchini na kimataifa. Sampuli tajwa ilitumiwa kuteua wasailiwa. Nadharia ya ubaada ukoloni iliwaongoza mtafiti kubainisha vipengele vya umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi. Hatimaye data iliokusanywa iliwasilishwa kuititia maelezo ya kifafanuzi na mifano. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa: Nyimbo za harusi mionganii mwa Wanandi kwenye runinga ya Kass zina vipengele vingi vya utamaduni wa jadi katika jamii ya Wanandi. Vilevile, nyimbo hizo zina baadhi ya vipengele vigeni hasa vinavyochangiwa na teknolojia na mwingiliano baina ya Wanandi na jamii zingine. Kadhalika umahuluti wa utamaduni umesaidia nyimbo za harusi mionganii mwa Wanandi kutekeleza majukumu yake katika jamii ya sasa. Kwa hivyo, utafiti huu ni muhimu kwa taaluma ya fasihi simulizi na vyombo vya habari hasa kwa wale walimu na wanafunzi watakaotaka kufanya utafiti wa suala la dhima ya umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi kwenye jamii za kiafrika.

UTANGULIZI

Utawala wa Wakoloni uliwaathiri watu katika koloni zao kiuchumi, kijamii na kisiasa. Zaidi ya hayo, mabadiliko katika utamaduni wa watawaliwa yalishuhudiwa katika fasihi andishi, Sanaa ya uchoraji na muziki. Nettl (2010) anadokeza namna tatu ambayo husababisha umahuluti wa utamaduni katika muziki kwenye kazi yake ya *Cultural Grey Out. (The Study of Ethnomusicology, 347-348)*, Kwanza ni msimamo mkali wa kuhakikisha utamaduni asili hauathiriwi na ule wa Magharibi, pili ni kuiga utamaduni wa Wakoloni kabisa na tatu ni kuchanganya tamaduni zote mbili hasa kwa kutumia teknolojia na miundo ya muziki ya hao Wakoloni huku watawaliwa wakihakikisha kuwa utamaduni wao asili haupotei. Hivyo basi uhakiki wa dhana ya umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi unapaswa kuhusisha uchambuzi wa vipengele vya utamaduni wa kale na ule geni; ambapo tamaduni hizo mbili zikiwepo ni ishara ya umahuluti wa utamaduni.

Dhana ya umahuluti wa utamaduni imeshughulikiwa sana na waandishi na hata wataalamu wengi wa baada ya ukoloni ulimwenguni. Wao wameeleza umahuluti katika muktadha wa utawala wa wakoloni na watu katika koloni zao. Wakati huo huo wamedokeza kuwa umahuluti wa utamaduni unahusu masuala ya mtagusano wa utamaduni na mabadiliko katika kazi za fasihi hasa yanayopinga kaida za Wakoloni. Hata hivyo, dhima ya umahuluti wa utamaduni katika kuhakikisha kuwa fasihi za baada ya ukoloni zinatekeleza majukumu yao haijashughulikiwa kikamilifu hivyo kuwa pengo ambalo lilishughulikiwa na utafiti huu kupitia uchunguzi wa nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi kwenye runinga ya Kass.

Kadhalika, wataalamu mbalimbali wamejaribu kutoa fasiri ya umahuluti wa utamaduni. Bhabha, (1994) ameelleza kuwa umahuluti wa utamaduni ni utamaduni wa tatu unaobuniwa baada ya utamaduni wa watawaliwa kutagusana na ule wa Wakoloni. Utamaduni huo wa tatu hupinga kaida za Wakoloni. Yazdiha (2010:35) amefananisha utamaduni na msafiri ambaye katika safari yake hukusanya mila na desturi za watu wanaotagusana nao njiani. Maelezo ya Yazdiha aidha yanafanana na ya

Bhabha (nimeshawataja) wakati anadokeza kuwa, umahuluti wa utamaduni ni namna moja ambayo watawaliwa wanapinga utawala wa Wakoloni hasa unaoenezw na lugha. Isitoshe, Kraudy (2002) amefafanua umahuluti katika muktadha wa mawasiliano kwa kueleza kuwa umahuluti wa utamaduni ni jinsi wenyeji hupokea matini kutoka vyombo vya habari ulimwenguni na kutoa nafasi nzuri ya mwingiliano wa utamaduni. Madai ya Kraudy yanaweka wazi nafasi ya vyombo vya habari katika kupalilia umahuluti wa utamaduni.

Kwa upande mwingine, waandishi wa bara la Afrika wamefasiri umahuluti wa utamaduni kuwa, ni utamaduni uliotokea wakati Wakoloni walitagusana na Wafrika na hali hiyo ingali inaendelezwa na utandawazi katika Afrika huru (Ferusa, 2009). Hali hii imewafanya baadhi ya wataalamu kutoka Afrika kudai kuwa utambulisho wa Wafrika umeathiriwa na utamaduni wa Wakoloni kiasi cha Wafrika kuacha mila zao na kuiga ya Wakoloni. Mathalan, Ngugi Wa Thiong'o (1994), anawahimiza waandishi wa baada ya ukoloni barani Afrika kuandika kwa lugha zao za mama kama alivyofanya ili kupinga kaida za Wakoloni; ambao waliwafunza Wafrika lugha za kigeni ili kuwafanya waache mila zao. Hata hivyo, Achebe (2006) ana maoni tofauti kwani aliandika riwaya ya *Things Fall Apart* akitumia Kiingereza ambacho kinaonyesha wazi utamaduni wa Nigeria. Achebe anadai kuwa mchango wa Wakoloni hasa kupitika lugha zao hauwezi kupuuzwa kwani umechangia maendeleo katika bara la Afrika.

Uchunguzi wa dhana ya umahuluti wa utamaduni barani Afrika hasa Kenya unaonyesha kuwa dhana hii imeshughulikiwa sana katika fasihi andishi hasa na waandishi wa tamthilia na riwaya ili kukashifu tabia za ukengeushi wa Wafrika na kuwashimiza Wafrika wasiache mila zao asili. Umahuluti wa utamaduni hata hivyo umepuuzwa katika tafiti zinazolenga fasihi simulizi inayoendelezwa na vyombo vya habari. Matei (2011) anahoji kuwa fasihi simulizi imebadilika hasa kwa sababu ya athari za Wakoloni na teknolojia iliyoletwa na Wakoloni ili kuendeleza utawala wao. Hata hivyo, fasihi simulizi ingali inatekeleza majukumu yake.

Nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi zinazidi kuonyesha umahuluti wa utamaduni hasa kupiticia mtindo. Nyingi ya nyimbo hizo kwa mfano, zina

matini ya dini ya Kikristu; jambo ambalo linaonyesha utamaduni wa Wakoloni kwani walitumia dini kama mbinu ya kiutawala (Korir, 2013). Kando na mtindo, kuna uwezekano wa nyimbo hizo kuwa na vipengele vingine vya umahuluti wa utamaduni. Hivyo basi lengo la utafiti huu ni kubainisha dhima ya vipengele hivyo vya umahuluti wa utamaduni.

Isitoshe watafiti aliona haja ya kuchunguza nyimbo za harusi katika kipindi mahususi kwenye runinga kwa sababu kuna uhusiano mkubwa kati ya utamaduni na utandawazi (Pieterse, 1996). Vyombo vya habari hasa runinga vimefanya dunia kuwa kama kijiji. Licha ya vituo vya runinga nchini Kenya kuwa na filamu kutoka nchi za Magharibi, vimekuwa mstari wa mbele katika kuhifadhi fasihi simulizi. Mathalani, vituo vya Citizen, NTV, KTN, KU TV na Kass huwa na vipindi vya harusi. Runinga ya Kass ilichaguliwa katika utafiti huu kwa sababu utafiti unahusu jamii ya Wanandi na kama anavyodai Matei (2011), kila Jamii huwa na nyimbo zake. Kadhalika runinga ya Kass ilikuwa runinga ya kwanza kutangaza kwa lahaja ya Kinandi na imekuwa ikipeperusha harusi miongoni mwa Wakalenjin hasa zenye nyimbo pendwa kwa zaidi ya miaka miwili. Nyimbo hizo zilichanganuliwa na utafiti huu ili kubainisha iwapo zinatekeleza majukumu yaliyokuwa yakitekeleza kabla ya Wanandi kutagusana na Wakoloni.

MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia ambayo ilitumiwa katika utafiti huu ni ile ya ubaada ukoloni. Njogu na Chimera (2008) wamefanua kuwa nadharia ya ubaada ukoloni inatumika kutoa maelezo ya uhusiano uliopo kati ya mataifa yaliyotawala na yaliyotawaliwa kwa sababu ya ukoloni. Wao wanasisitiza kuwa nadharia hii hueleza athari za ukoloni katika utamaduni, uchumi na siasa hata baada ya nchi zilizotawaliwa kupata uhuru wa bendera. Wanazuoni hawa wanaeleza kuwa nadharia hii inaweza kutumika katika uchambuzi wa kazi kadha za fasihi. Jambo ambalo ni muhimu kwa mtafiti ni kutambua kuwa, lugha ni kielelezo cha utamaduni; hivyo hana budi kuchunguza athari za tamaduni zingine katika lugha asili. Madai haya yalikuwa nguzo kwetu kwani tulitaka kuweka wazi vipengele vigeni kwenye nyimbo za harusi baada ya lugha ya mkoloni kuingiliana na ya Wanandi. Hatimaye

kudhihirisha namna vipengele hivyo vianasaidia nyimbo hizo kutekeleza majukumu yake katika jamii yenyе umahuluti wa utamaduni.

Dhana ya umahuluti wa utamaduni imefafanuliwa kwenye nadharia ya ubaada ukoloni na wanazuoni kama vile: Bill Ashcroft, Edward Said, Homi Bhabha, Gayatri Chakravorty Spinak na Robert Young. Dhana hii ina historia ndefu. Katika kazi yake ya *Colonial Desire: Hybridity. Theory, Culture & Race*, Young (1995) anafafanua kwamba dhana ya umahuluti imechimbuka kutoka bayolojia. Dhana hii inarejelea ubaguzi wa rangi kwani kizazi kilichozaliwa kutokana na uhusiano wa farasi na punda hakikuwa na uwezo wa kuzaa. Hivyo basi, katika enzi za kikoloni, ndoa kati ya Wakoloni na Watawaliwa ilishutumiwa kwa sababu umahuluti huo wa utamaduni ulirejelea madai ya dhana hii katika bayolojia. Kadhalika, Young (nimeshamtaja) anaonyesha matumizi ya dhana ya umahuluti wa utamaduni katika nadharia ya ubaada ukoloni kuwa, unahusu utamaduni bali si ubaguzi wa rangi. Mwanazuoni huyu anaeleza kuwa kila utamaduni hubadilika kutoka hali yake asili hadi kuwa mahuluti kwa sababu ya kukopa vipengele vya tamaduni zingine. Hata hivyo, Young anasisitiza kuwa jamii tofauti zikitagusana hukopa vipengele chanya vya utamaduni mgeni.

Kulingana na mwanafilosofia wa Ujerumani Johann Gottfried Herder aliyenukuliwa na Young, maendeleo ya binadamu yanatokana na mwingiliano wa utamaduni na mawasiliano; ambapo maendeleo ya utamaduni mmoja yanaingia kwa mwengine. Mwanafilosofia huyu anatoa mfano wa Uingereza ambapo japo imeendelea, imekopa utamaduni wa Warumi, Waarabu na Wayahudi hasa katika hesabu na dini. Madai haya yanatilia mkazo lengo la tatu la utafiti huu; ambalo kutokana na Wanandi kuingiliana na Waingereza, nyimbo zao za harusi zimeathiriwa na utamaduni wa Waingereza. Hata hivyo nyimbo hizo zingali zinatekeleza majukumu yao jambo ambalo linaoyesha mchango wa umahuluti wa utamaduni.

Mwanazuoni anayeaminiwa kuwa aliipa mashiko nadharia ya ubaada wa ukoloni ni Edward Said kwenye kitabu chake cha Orientalism (1978) Utafiti huu uliona haja ya kurejelea kazi kwenye kitabu hiki wa sababu inatueleza kuhusu utabaka uliotokea kati ya nchi za mashariki (mfano Afrika) na

Magharibi (mfano Uingereza). Dhana ya umashariki inaonyesha kuwa kazi zote za kitaaluma zinadunisha mataifa ya mashariki Kenya ikiwemo, kuwa zimebaki nyuma katika dini, siasa, uchumi, elimu na kiteknolojia. Yaani hazijastaarabika. Madai ya Edward Said kwenye kitabu hiki kinaonyesha kuwa kuna ukuta au pengo kubwa kati ya Wakoloni na Watawaliwa hivyo kupinga nafasi ya umahuluti wa utamaduni. Hata hivyo, miaka kumi na sita baadaye, Edward Said anatoa mchango tofauti kwenye nadharia ya baada ya ukoloni katika kitabu chake cha *Culture and Imperialism* (1994). Mwasisi huyu anapuuza dhana ya utabaka kati ya Wakoloni na Watawaliwa na kudai kuwa tamaduni zote zinategemeana na hakuna utamaduni ambaeo hauna athari za tamaduni zingine. Anasisitiza kuwa tamaduni zote ni mahuluti. Pia anaongeza kuwa utamaduni wowote hukubali vipengele vigeni badala ya kuvikataa. Mwanazuoni huyu sawa na Homi Bhabha anapinga ubepari kwa kuhimiza utamaduni wenyewe usawa kupitia umahuluti wa utamaduni. Mawazo haya ni muhimu katika utafiti huu ambaeo unaamini kuwa nyimbo za Wanandi zina vipengele vigeni kutoka kwa Waingereza na jamii zingine za kiafrika.

Nikiongezea, mchango wa Homi Bhabha katika dhana ya umahuluti ni wa kupigiwa mfano. Anadai kuwa umahuluti wa utamaduni unapaswa kueleweka kama wakati ambapo utawala wa Wakoloni unakandamizwa ili kutoa nafasi ya kutambuliwa kwa mila, desturi na lugha ya Watawaliwa (1994). Hivyo basi, Bhabha anatetea usawa wa utamaduni kupitia umahuluti wa utamaduni. Katika maelezo yake, Bhabha anaonyesha namna umahuluti wa utamaduni huhoji mifumo za kikoloni kupitia ukandamizaji, udunishaji wa mila na lugha za Watawaliwa. Aidha anapendekeza kuwa umahuluti ni mchakato wa kukataa dhuluma za ubepari dhidi ya utamaduni wa jadi wa Wafrika. Kwa kweli mawazo haya yanaonyesha kuwa umahuluti wa utamaduni hutoa nafasi nzuri ya kukosoa na kupinga utamaduni wa Wakoloni (1994). Mawazo haya ya Bhabha (nimeshamtaja) yatatumiwa kuhakiki vipengele vya jadi kwene nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi; ambavyo vinaonyesha namna wasanii wa sasa wamehifadhi utamaduni wao licha ya kuwa sherehe ya harusi ina asili yake katika utamaduni wa Wakoloni.

Isitoshe, Bhabha anadai kuwa umahuluti wa utamaduni ni nafasi nzuri ya kutagusana kwa utamaduni wa asili na wa Wakoloni. Katika kitabu chake cha *The Location of Culture* (199) anataja kuwa kukubali tofauti za utamaduni na kukataa dhana ya kuwepo kwa utamaduni ulio bora zaidi ni namna moja ya kuhimiza umahuluti wa utamaduni. Kwa hivyo umahuluti wa utamaduni utatokea palipo na mwngiliano wa tamaduni mbili ili kuondoa utabaka. Yaani kwa lugha wazi ni kuwa umahuluti wa utamaduni ni hali ya kukataa mifumo ya utawala wa Wakoloni. Mfano mojawapo ya mifumo ya Wakoloni inayokataliwa kwenye baadhi ya nyimbo zitakazohakikiwa kwenye utafiti huu ni taasubi ya kiume.

Dhana ya ukengeushi na nafasi ya tatu imefanaliwa pia na Bhabha kwenye nadharia ya ubaada ukoloni. Ukengeushi (mimicry) kulingana na Bhabha ni hali ya kuiga tabia za wakoloni. Ukengeushi ultokea kabla na baada ya ukoloni. Namna moja ya kuonyesha kuwa mhusika fulani amekengeuka katika mazingira ya nchi ya Kenya ni kutumia lugha ya Kiingereza. Uhakiki wa nyimbo katika sampuli yetu utachunguza dhana hii kwa kina. Nafasi ya tatu kulingana na Bhabha (nimeshamtaja) ni utamaduni unaotokea wakati ambapo kuna mwngiliano kati ya utamaduni wa mkoloni na wa Watawaliwa wake. Utamaduni huo huwa tofauti na zile zilizoingiliana. Nafasi hiyo ya tatu inaweza kuelewsa kama ubunifu wa wasanii katika nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi.

Mchango wa Gayatri Chakravorty Spinak (1988a) hauwezi kupuuzwa katika nadharia ya ubaada ukoloni. Spinak anajiita Mfeministi Maksi na anaeleza namna nchi za magharibi zinadhibiti, nyanyasa na kunyakua rasilimali na mawazo kutoka mataifa yanayoendelea. Yeye (Spinak) anatetea wanawake wanaonyanyaswa katika mifumo ya ubabedume iliyoletwala na Wakoloni. Mawazo ya Spinak kwenye kitabu *The Construction of Knowledge from the West* yanaona na yale ya Edward Said kuwa ulimwenguni, mataifa yanayoendelea hubuni maelezo yanayohusu mataifa ya Mashariki kuwa masomo ya kijamii yanayohusu mataifa yanayoendelea huandaliwa na kusambazwa kote ulimwenguni kupitia teknolojia. Maoni haya ya Spinak yatatuelekeza katika kuchunguza nafasi ya mwanamke kwenye nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi.

Hatimaye, Bill Ashcroft, (2001) katika mabadiliko ya baada ya ukoloni anaeleza kuwa, tafiti za baada ya ukoloni zilichimbuka kama namna ya kujishughulikia matatizo yaliyoyakumba jamii zilizotawaliwa na wakoloni. Anaeleza kuwa japo ukoloni ulikuwa mfumo wa kukandamiza, ulikuwa na mchangano chanya kama vile: ujenzi wa shule, kanisa, hospitali na barabara ambayo iliwasaidia WaAfrika kutagusana na watu wa tamaduni zingine ulimwenguni. Athari chanya anazorejelea Bill zinaweza kutambuliwa katika nyimbo za kitamaduni ambazo nyingi zimesalia kwa sababu ya kuhifadhiwa na kusambazwa kupitia vyombo vya habari. Isitoshe, uwasilishaji wa nyimbo hizo umehimarishwa kupitia ala za muziki za kisasa.

Aidha, Bill Ashcroft (2001) anaeleza kuwa utamaduni hubadilika ili ustahimili mabadiliko katika jamii. Mabadiliko hayo hata hivyo hutokea wakati kuna mwingiliano wa tamaduni mbili au zaidi. Katika mwingiliano huo, utamaduni asili katika tamaduni zote zinazoingiliana hypotea ili kutoa nafasi ya umahuluti wa utamaduni. Imani ya Ashcroft ni kuwa utamaduni wa Wakoloni haukuharibu utamaduni asili wa WaAfrika kwa kudai kuwa WaAfrika wakilalamikia athari za ukoloni kwa utamaduni wao; hivyo basi watakataa maendeleo yoyote yaliyoletwa na mataifa yaliyoendelea. Mwingiliano wa Wakoloni na Watawaliwa unatoa nafasi nzuri ya umahuluti wa utamaduni ambao unaleta maendeleo katika jamii. Maoni ya Bill Ashcroft yanadhihirika wazi kupitia ustaarabu unaoshuhudiwa Afrika na hasa namna nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi zimepiga hatua katika mtindo, maudhui na utendaji baada ya Wanandi kuingiliana na Wakoloni

Dhana ya umahuluti wa utamaduni imekua kutegemea mpwito wa wakati na kuhusishwa na taaluma zingine. Mathalani, Yazdiha (2010) na Kraidy (2002) wamechangia ufanuzi wa dhana ya hii hasa katika dunia ya utandawazi. Yazdiha (2010) anapendekeza kuwa umahuluti unaweza kutumiwa kama silaha ya kupinga kaida za lugha. Yaani ni namna ya kubuni miundo mipya ya kukosoa mifumo zinazoendelea utabaka. Mawazo haya yanashabiana na ya Bhabha kama nivyooleza hapo awali. Kraidy (2002) anaeleza kuwa umahuluti ni dhana elezi inayofanua namna watu wa eneo fulani hupokea habari za dunia na kusababisha mtagusano wa utamaduni. Ufanuzi

wa Kraidy (nimeshamtaja) unaonyesha kuwa umahuluti ni zao la mwingiliano wa utamaduni wa ulimwengu na ule wa jamii mahususi. Mawazo haya yanaonyesha mchangano wa vyombo vya habari katika kuendeleza umahuluti wa utamaduni. Baada ya kueleza dhana ya umahuluti wa utamaduni kama ilivyofafanuliwa na wanazuoni mbalimbali utafiti huu uliteua mihimili ifuatayo ili iwe misingi ya uhakiki wa data kwenye sampuli za nyimbo zilizoteuliwa.

Hakuna utamaduni unaochimbuka na kuendelea kivyake bali lazima ikope kutoka tamaduni zingine kadri jamii inavyobadilika. Utafiti huu ultumia mhimili huu kubainisha dhima ya umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi. Pili ni kuwa, Shughuli za kikoloni ziliathiri utamaduni wa Watawaliwa hasa lugha za asili. Mhimili huu utatumwa kuchunguza maneno ya Kiingereza ambayo yanajitokeza katika sampuli ya nyimbo zilizoteuliwa. Tatu ni kwamba, kazi za fasihi mionganoni mwa WaAfrika zinadhahirisha hali ya kupinga mifumo ya kiutawala iliyoletwa na Wakoloni. Mhimili huu ultumiwa hasa kuchunguza kipengele cha utamaduni wa jadi katika sampuli ya nyimbo zilizoteuliwa; ambavyo vikichunguzwa kwa kina vinaonyesha kuwa Wanandi wanauenzi utamaduni wao asili na wanapinga tabia ya kuiga utamaduni wa Wakoloni. Pia mwingiliano wa utamaduni wa Wakoloni na Watawaliwa ulisababisha zao la utamaduni wa tatu ambao una vipengele vya tamaduni zote mbili lakini haufanani na wowote ule. Mhimili huu utatumwa kuhakiki vipengele vya utamaduni geni kwenye sampuli ya nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi. Hatimaye, umahuluti wa utamaduni huchochea ubunifu mionganoni mwa wasanii na kusababisha kuzuka kwa mitindo mipya kwenye kazi za fasihi; ambayo hukosoa kaida za Wakoloni. Mhimili huu utatumwa kuhakiki mitimdo mipya katika nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi.

DHIMA YA UMAHULUTI WA UTAMADUNI KATIKA UAMILISHAJI WA NYIMBO ZA HARUSI

Uchanganuzi wa sampuli ya nyimbo sita za harusi zilizoteuliwa kimaksudi kutoka kipindi cha Tumdo katika runinga ya Kass, ulibainisha kuwa umahuluti wa utamaduni una umuhimu anuai.

Kuhifadhi na Kuendeleza Utamaduni

Dhima kuu ya umahuluti wa utamaduni ni kuhakikisha kuwa utamaduni wa jadi haupotei. Hii ni kwa sababu, watanzi wanauhaisha huo utamaduni kupitia kwa nyimbo ili kizazi cha leo kijue yaliyotendeka hapo jadi. Tukizingatia mfano wa ujumbe kwenye wimbo wa *Tumin*, tunaelezwa kuhusu namna Wanandi wa jadi waliishi iwapo hawangejaliwa mtoto. Wao walipanga mtoto huyo kwa kumpa zawadi ya ng'ombe mwenye mtoto. Wasailiwa wa utafiti huu wanafafanua ujumbe huu kwa kusema kuwa, mume alisailiwa na kina babu huku mke akisailiwa na kina bibi ili kubainisha mwenye kasoro.

*Eng pitonab Kalenjin
Chi nekimakotinye lakwa ko kekanapchin
Ak kindechi kupesaik chich
Kotun kikochin tiondo bichotok*

Kando na mfano huu, utamaduni wa Wanandi umehifadhiwa kupitia sheria za ndoa kama ilivyo kwenye wimbo wa *Cheptab Oret Age*; ambapo mwanamke amehimizwa kuhusu majukumu yao katika ndoa. Tatu ni kupitia ujumi wa vifaa vya vibuyu na mavazi ya kitamaduni yaliyovaliwa na fanani au waimbaji wa nyimbo hizi za harusi. Watunzi wamevitumia vipengele vya jadi katika nyimbo za harusi ili kuhifadhi mila jambo ambalo linafasiriwa na wataalamu katika nadharia ya ubaada ukoloni kuwa; ni namna moja ya kupinga kaida za Wakoloni.

Kutambulisha Jamii

Nyimbo za harusi mionganini mwa Wanandi kwenye runinga ya Kass zinaimbwa kwa kutumia lugha asili ya Kinandi. Kwa mujibu wa Buliba, Njogu na Mwihaki (2006), lugha inaweza kufichua mengi kuhusu mtu. Mathalan, lugha ya Kinandi inafichua mazingira wanayoishi Wanandi na shughuli zao za kila siku. Wimbo wa *Asai* kwa mfano, inaeleza kuhusu ng'ombe wanaopelekwa zizini: *Kirot tich koba gaa* (ng'ombe wakapelekwa nyumbani). Aidha, kuwepo kwa matini ya biblia inaitambulisha jamii ya Wanandi baada ya Wakoloni kuwa wao wamekubali imani ya Kikristu.

Kando na lugha kuitambulisha jamii, vipengele vingine vya utamaduni kama vile: chakula, vifaa na

Baada ya usaili huo, kama mama ni tasa mume angeshauriwa kuoa na kama mume ni ghumba, mwanamume mwenye maadili mema angetafutwa kumpa watoto na baadae angepewa ng'ombe. Aidha mama tasa alipewa nafasi ya kununua mtoto na kulipa kwa ng'ombe. Hadi wa leo kuna watu mionganini mwa Wanandi ambaao inadaiwa walinunuliwa baada ya ‘mama zao’ kukosa watoto kwani walipoenda kuwatumikia wazungu kwenye mashamba yao, uzazi wao ulilemazwa na dawa za kupanga uzazi; ambazo wazungu waliwapa. Mistari ifuatayo inaelezea utamaduni huu:

*Katika jamii ya kale ya Kikalenjin
Mtu asiyejeliwa mtoto angepewa
Angewekewa mtoto huyo kwenye mapacha
Mwenye kutoa mtoto angepewa zawadi ya
mnyama (ng'ombe)*

mavazi huitambulisha jamii. Vipengele hivi vilijitokeza wazi kwenye kanda za wasanii na maneno yaliyotumiwa na wasanii. Kanda hizo zikitazamwa, mtu ye yeyote hutambua kuwa wimbo husika ni wa jamii ya Wanandi hata kama haelewi Kinandi. Dhima hii ya umahuluti wa utamaduni kuwa kitambulisho cha jamii ni kwa sababu Wafrika hupinga athari za utamaduni wa Wakoloni kwa kuhifadhi utamaduni wao wa jadi.

Jamii ya vijana inatambuliwa kupitia matumizi ya msimbo wa sheng'. Msimbo wa sheng ni mfano wa lugha mahuluti inayopinga mifumo sanifu za lugha ya kiutawala kama vile Kiswahili na Kiingereza. Mtunzi wa *Cheptab Oret Age* anatumia maneno *sistee na mathee* (dada na mama) ili kujitambulisha na vijana na wakati huo huo kupinga mfumo sanifu wa lugha ya Wakoloni (Kiingereza)

Kuondoa Vizingiti vya Mawasiliano

Mtagusano baina ya watu ulimwenguni umesababisha mwingiliano wa kitamaduni. Kwa mujibu wa Said (1994), utamaduni mmoja hukubali baadhi ya vipengele vya utamaduni geni badala ya kuvikataa kwani tamaduni zote hutegemeana. Mfano wa kipengele ambacho huathiri tamaduni zote ulimwenguni ni lugha. Kwa sababu ni vigumu sana kwa lugha asili kueleza dhana iliyo katika lugha ya pili, lugha asili hukopa maneno kutoka

lugha nyingine ili kuelezea mambo mapya. Mfano Wanandi wametumia maneno: *airport* na *dijital* kwenye wimbo wa *Asai* kwa sababu hawana istilahi za dhana hizi geni. Katika wimbo wa *Iyoni Ng'o Tumi*, Wanandi wametohoar harusi iwe *arusit* kwa sababu harusi ni jambo geni kwao.

Kadhalika, Wasanii hukopa maneno hasa ya kiingereza ili kushirikisha hadhira. Katika jamii ya sasa ambapo watu kutoka jamii mbalimbali ulimwengu wameingiliana, Lugha inayoelewaka na wengi mathalani Kiingereza ni daraja ya kuwaunganisha watu wote. Watu wengi nchini Kenya na ulimwenguni wanaelewa ujumbe wa kitiikio cha wimbo wa *Very Nice Tumdo*. Wimbo mzima na hata kununua kanda ya wimbo huo.

Kuziba Pengo la Upungufu wa Kiutamaduni

Kila utamaduni una upungufu wake. Mfano mzuri katika jamii ya Wanandi ala za kimuziki. Itakuwa vigumu sana kwa wasanii kutoka jamii ya Wanandi kutumia ala za kale za muziki katika jamii ya sasa yenye maendeleo ya kitenango. Matumizi ya piano kwenye nyimbo za harusi imewafanya nyimbo za harusi mionganii mwa Wanandi kuvutia na kushirikisha hadhira yote. Kando na ala za kimuziki, suala la uimbaji kutengewa jinsia ya kike pekee ilikuwa inawanyima nafasi wanaume kukuza talanta zao za uimbaji. Utandawazi hivyo basi, umewafanya Wanandi kubuni nyimbo zao na kuijiendeza kiuchumi huku wakichangia katika uhifadhi wa mila za jamii yao. Mfano wa mtunzi ambaye amefaidika kutona na umahuluti wa utamaduni ni Mwalimu Kendagor; ambaye utafiti huu ulirejelea nyimbo zake tatu: *Cheptab Oret Age, Leketyo na Tumin*. Nyimbo hizi ni maarufu sana mionganii mwa Wanandi na zina vipengele vya utamaduni wa jadi.

Kuburudisha

Jukumu mojawapo ya nyimbo katika jamii ya Wafrika kulingana na Matei, (2011) ni kutumbuiza. Jukumu hili halijabadilika bali umahuluti wa utamaduni umeliboresha. Mathalani, densi za jadi mionganii mwa Wanandi zilikuwa mithili ya mwendo wa ng'ombe. Densi hizi aidha zilikuwa za akina mama na wasichana peke. Umahuluti wa utamaduni hasa midundo ya ala za muziki imewafanya Wanandi kukopa mitindo mingine ya

densi hasa kutoka kwa Waluyha, Wamasai na Wamarakwet. Kila mtu kwenye harusi hucheza wakati ambapo wimbo fulani umechezwa. Hii inathibitisha namna ala geni za muziki huwa chachu ya burudani. Aidha, Wanandi kuacha mila ya kuwapa wanawake peke jukumu la kushiriki kwenye nyimbo za harusi imeisaidia hadhira yote kufurahia wimbo husika

Kukuza Ubunifu Mionganii mwa Wanajamii

Nyimbo ambazo zilitaaliwa kwa kipindi cha *Tumdo* kwenye runinga ya *Kass* ni mali ya watu binafsi kinyume hapo awali; ambapo fasihi simulizi ilikuwa mali ya jamii. Hali hii ya kubinafsishwa kwa fasihi imewafanya watunzi wa nyimbo za harusi kuteua maneno kiufundi ili nyimbo zao zipendwe si tu na Wanandi bali jamii zingine. Ubunifu huu unajitokeza kupitia mtindo wa kurejelea matini ya biblia, hurafa, mighani na mawaidha ya sheria za ndoa kwenye nyimbo za harusi. Ubunifu pia unajidhihirisha wakati ambapo wasanii wanakopa maneno ya kiingereza au Kiswahili ili kuwasilishia ujumbe ambao haungeimbika vyema iwapo Kinandi kingetumiwa. Kwa mfano tafsiri ya mstari *very nice tumdo* ni *kararan netia tumdo*.

Ifahamike kuwa, umahuluti wa utamaduni husababisha ubunifu mionganii mwa wanajamii kulingana na nadharia ya ubaada ukoloni. Mawazo haya yanatiliwa mkazo na namna watunzi wa Nyimbo za harusi mionganii mwa Wanandi waliteua vifungu vya biblia viliviyolenga kutoa mafundisho ya ndoa peke. Kwa mfano wimbo wa *Kapchi, Iyoni Ng'o Tumi* na una mistari inaonya wanaharusi didhi ya talaka kama ilivyo kwenye mafundisho ya biblia. Kifungu hicho cha *chekakituyo komebestos chi* chenye maana ya waliounganiswa mwanadamu asiwatenganishe kinaoana na mafundisho ya Wanandi kuhusu talaka.

Kupanua Muktadha wa Matumizi ya Nyimbo

Nyimbo za harusi mionganii mwa Wanandi haziimbwi tu katika muktadha wa harusi kinyume na hapo jadi. Hii ni kwa sababu nyimbo hizo zimetungwa kwa ufundi wa hali ya juu. Athari ya dini ya Kikristu inajitokeza wazi kwenye maudhui ya dini na matini ya biblia. Kuwepo kwa maudhui

haya ya dini ya Kikristu kunafanya nyimbo hizo kuimbwa kanisani. Mfano wa wimbo unaoweza kuwa wa kidini vilevile ni ule wa *Kapchi* ambao ultungwa na Mum Cherop. Isitoshe, wimbo wa *Very nice tumdo* unawenza kuimbwa katika sherehe yoyote yenye toni ya furaha. Kwa mfano tarehe 21/6/19, wimbo huo ultumiwa kuburudisha wageni katika sherehe ya kufungua kiwanda cha *Rivatex* kule *Eldoret*. Kwa sababu neno *tumdo* lina maana ya sherehe mionganoni mwa Wanandi, kuongeza kivumishi cha Kiingereza *Very nice* kunafanya wimbo huo kuimbwa popote isipokuwa kwenye mazishi.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Katika nakala hii, tumewasilisha, kujadili na kufasili data ya utafiti wetu ili kutimiza malengo ya utafiti wetu. Tumevibainisha vipengele vyaya jadi na vigeni kwenye sampuli ya nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya ubaada ukoloni iliyoteuliwa katika utafiti huu. Hatimaye tumbainisha dhima ya umahuluti wa utamaduni katika nyimbo za harusi mionganoni mwa Wanandi ili kutimiza lengo la tatu la utafiti wetu.

Umahuluti wa utamaduni ni dhana ambayo haiwezi kuepukwa katika jamii ya sasa. Hata hivyo, kuna haja ya watunzi wa nyimbo za utamaduni wa asili nchini Kenya kutumia umahuluti wa utamaduni kwa uangalifu ili kurithisha kizazi cha leo na kesho utamaduni wa jadi. Watunzi wakifanya hivyo, Umahuluti wa utamaduni utakuwa na manufaa mengi katika kuhakikisha kuwa nyimbo za harusi zinatekeleza majukumu yake.

MAREJELEO

Achebe, C. (2006). The Politics of Language. In B. Ashcroft, G. Griffiths, & H. Tiffin: *The Post-colonial Studies Reader* (pp. 268-271). Oxford: Routledge.

Bhabha, H. (1994). *The Location of Culture*. London: Routledge.

Bill, A. (2001). *On Post-Colonial Futures: Transformation of Colonial Culture*. London: Routledge.

Buliba, A., Njogu, K., na Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ferusa, M. (2009). Theorizing Through African Literature: Bridging the Gap between Individuality & Sociality. *Paper Presented at the Annual Meeting of the 33rd Annual National Council for Black Studies Renaissance*. Atlantan Hotel Downtown, Atlanta, GA, Maria.

Korir, J. (2013). *Appropriation of Kipsigis Idiom in Selected Gospel Songs of Joel Kimeto*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kraudy, M. (2002). Hybridity in Cultural Globalisation. *Communication Theory*. 12 (13), 316-319

Matei, A.K. (2011). *Fani za Fasihi Similizi*. Nairobi: Oxford University Press.

Nettl, B. (2010). *Nettl's Elephant: On the History of Ethnomusicology*. Urban: University of Illinois Press

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008) Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

Pieterse, J. N. (1996). *Globalization as hybridization*. London: Sage

Said, E. (1978). *Orientalism*. New York: Panthem.

Said, E. (1994). *Culture and Imperialism*. New York: Knopf.

Spinak, G. C. (1988). Can the Subaltern Speak? In C. Nelson & L. Grossberg (eds), *Marxism and The Interpretation of Culture*. Urbana: University of Illinois Press.

Wa Thiong'o, N. (1994) The Language of African Literature: In P. Williams & L. Chrisman, *Colonial Discourse and Post-Colonial Theory Reader* (pp. 435-456). New York: Columbia University Press

Yazdiha, H. (2010). Conceptualizing Hybridity: Deconstructing boundaries through the hybrid. *Formations* 1 (1), 31-38.

Young, R. C. (1995). *Hybridity in Theory, Culture and Race*. London: Routledge